**FORM FOUR CLUSTER KCSE MODEL9**

**KISWAHILI PAPER 3 QUESTIONS**

## 1.SEHEMU A: (Alama 20 )

**USHAIRI**

1. **LAZIMA**

Soma shairi hili kasha ujibu maswali.

Sanya J.Situma: Ovasia

**DARAJA -1116 J**

**OVASIA –Mtunzi Bw. Sanya J. Situma**

Najitia uwanjani,fumbo kufumbua.
Mambo haya ya kihuni,twayaona maridhia.
Twayatia akilini,macho kupofua.
Ndugu yangu ovasia. faraghani wafanyani?

Juzi juzi kanisani,ulikuwa mtubia.
Ukatiwa kidimbwini,dhambi zako kuzivua.
Leo hino uwewini,na kashinda wavalia.
Ndugu yangu ovasia. faraghani wafanyani?

Mbinu tele umebuni,waumini kuhadaa.
Ja sauti yenye shani,nazo mbwembwe za bandia.
Bibilia mkononi,ukaisi umetwaa.
Ndugu yangu ovasia. faraghani wafanyani?

Intaneti washeheni,wahisani kuvutia.
Picha zao masikini,mtandaowajazia.
Wajificha mvunguni,misaada 'kipokea.
Ndugu yangu ovasia. faraghani wafanyani?

Runingani,redioni,la mkazo watilia.
''mbegu tele zipandeni,ja magari na rupia''.
Matoleo wathamini,kuipiku injilia.
Ndugu yangu ovasia. faraghani wafanyani?

Kwayo mali ulohini,siaisani wanyatia.
Kusambaza uumini,hivyo ndivyo wadaia.
Wafikiri hatuoni,hila zako za tama?
Ndugu yangu ovasia. faraghani wafanyani!

Nimefika ukingoni,yangu rai naitoa.
Masihara tuwacheni,kwalo neno la Molia.
Kazi moja hifadhi,robo tele kuokoa.
Ndugu yangu ovasia. faraghani wafanyani?

a) Ainisha kwa ithibati utungo huu katika bahari mbili. (alama2)
b) Huku ukitoa mifano,eleza dhima ya aina mbili za idhini ya ushairi katika shairi hili. (alama4)

c) Mtunzi wa utungo huu ana ujumbe gani kwa wanajamii? (alama2)

d) Bainisha toni ya nafsineni. (alama2)

e) Tambua kwa mifano tamathali zozote tatu za usemi ambazo zimetumiwa. (alama3)

f) Falsafa ya mtunzi wa shairi hili ni nini? (alama2)

g) Andika tafsili ya ubeti wa saba. (alama4)

h) Fafanua kifungu 'ukatiwa kidimbwimbwi,dhambi zako kuzivua'. (alama1)

## 2. SEHEMU B: (Alama 20 )

**TAMTHILIA**

2. **T.Arege:Mstahiki Meya.**

. ''….tuyafanye maneno yote ya Cheneo kuwaka moto wa mafanikio….Kumbuka kila kilio kina maana yake!''

a) Liweke dondoo hili katika muktadha unaofaa. (alama4)

b) Fafanua chanzo cha 'kilio' kinachorejelewa katika nukuu. (alama10)

c) Eleza mbinu zozote nne hasi ambazo zimetumiwa na utawala wa Cheneo kukomesha kilio hicho. (alama4)

d) Kuna tamathali mbili za lugha ambazo zimetumiwa katika dondoo hili.Thibitisha. (alama2)

3. Jamii ya Mtahiki Meya imeathiriwa vibaya na ufisadi uliokithiri.Jadili.

## 3. SEHEMU C: (Alama 20 )

**RIWAYA**

4. **K.Walibora :Kidagaa Kimemwozea.**

**Jibu swali la 4 au la 5 4.**

''Kama huyu ni mwanangu basi nilizaa na nani?Pasi ya viganja viwili kofi hazilii''.

a) Tambua mnenaji na mnenewa wa dondoo hili. (alama2)

b) Bainisha tamathali mbili ambazo zimejitokeza katika usemi huu. (alama4)

c) Kwa kurejelea kisa cha dondoo,eleza udhaifu wa msemewa. (alama14)

5. . Jadili majukumu yoyote kumi ya vijana katika jamii kwa mujibu wa riwaya Kidagaa Kimemwozea.

## 4. SEHEMU D: (Alama 20 )

**HADITHI FUPI**

6. **K.Walibora na S.A Mohammed**

**:Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine.**

**Jibu swali la 6 au la 7 Shaka ya Mambo (F.Topan)**
Hadith; Shaka ya Mambo ni shaka ya mambo kweli.Jadili. (alama20)

'Mwana wa Darubini''.(K.M Mbai)

7. ''Hata hivyo kadiri walivyomsikiliza ndivyo walivyomwelewa….'

a) Liweke dondoo hili katika muktadha faafu. (alama4)

b) Eleza jinsi msemwa alivyokabiliana na changamoto katika maisha yake. (alama16)

## 5.SEHEMU E: (Alama 20 )

### FASIHI SIMULIZI

8. a) Eleza dhima nne za hojaji katika utafiti wa fasihi simulizi. (alama4)

b) Fafanua vizisingizi vyovyote vinane katika ukusanyaji wa fasihi simulizi. (alama16)